


# Kuongoza Mafunzo

## Muhtasari wa taarifa ya uongozi fanisi na elimu bora Zanzibar

THE REVOLUTIONARY GOVERNMENT
OF ZANZIBAR MINISTRY OF EDUCATION
AND VOCATIONAL TRAINING

VSO

# Historia

Zanzibar imepiga hatua kubwa ili kufikia lengo lake la 'Kujitahidi kuleta upatikanaji sawa wa elimu bora kwa wote na kuendeleza mafunzo ya kudumu katika utoaji elimu tangu ilipopata Mapinduzi yake mwaka 1964. Miaka kumi iliyopita, upatikanaji wa elimu ya msingi na ya sekondari uliongezeka sana na Zanzibar iko njiani kufikia lengo la Maendeleo ya Milenia katika uandikishaji halisi wa skuli za msingi. Mkazo zaidi sasa unawekwa katika mchakato wa kufundisha na kujifunza maskulini na matakwa ya 'elimu bora kwa wote na kuendeleza mafunzo ya kudumu.'

> "Kujitahidi kuleta upatikanaji sawa wa elimu bora kwa wote na kuendeleza mafunzo ya kudumu."
>
> *Tamko la Lengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA)*

WEMA inaona uongozi wa skuli wenye ufanisi kuwa jambo muhimu katika kuendeleza mabadiliko ya elimu na kuinua viwango vya matokeo ya wanafunzi. Mfumo wa elimu wa Zanzibar unaelekea kutoa madaraka kwa ngazi za chini ili kusaidia matokeo bora katika ngazi ya darasa. Kwa walimu wakuu, madaraka katika ngazi ya chini itamaanisha kutoka katika wajibu wa utawala zaidi kwenda katika wajibu wa uongozi. Wakuu kupewa madaraka na kusaidiwa kufanya mabadiliko haya litakuwa jambo muhimu kwa kuendeleza ubora. Uongozi fanisi wa skuli ni muhimu kwa utoaji wa elimu bora na mafunzo ya kudumu. Utafiti wa 'kuongoza mafunzo' ulichunguza uhusiano kati ya uongozi wa skuli na ubora wa elimu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

Utafiti wa 'kuongoza mafunzo' ulichunguza uhusiano kati ya uongozi wa shule na ubora wa elimu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

- Elimu bora humaanisha nini kwa watu wa Zanzibar?
- Sifa binafsi na matendo ya Mwalimu Mkuu fanisi Zanzibar ni yapi?
- Ni mabadiliko gani ya msingi yatakayowawezesha walimu wakuu kuongoza mabadiliko katika elimu na kuinua viwango vya matokeo ya wanafunzi?

Taarifa hii ni matokeo ya mradi wa utafiti wa miezi kumi na nane uliotekelezwa baina ya WEMA na VSO Tanzania chini ya usimamizi wa Kamishina wa Elimu. Utafiti ulioendeshwa na Martin Brown na Yasmin Ajmal, wataalamu wawili walioajiriwa na WEMA kutoka shirika la VSO. Watu 270 walishiriki katika utafiti huu wakiwemo; watoto, wazazi, walimu, Walimu wakuu, Maafisa Elimu wa Wilaya, Wakaguzi, wawakilishi wa Kituo cha Taifa cha Walimu na Maafisa wa WEMA kutoka Unguja na Pemba.

## Elimu bora

Wazazi, wataalamu wa elimu na wanafunzi mara nyingi huweka mikazo tofauti katika dira zao za elimu bora. Wazazi kwa ujumla hupima ubora kuhusiana na matokeo ya elimu kama vile kazi na fursa za maisha za watoto wao, wataalamu wa elimu huelekea kuonyesha haja ya vifaa bora kama vitabu vya kiada, wakati wanafunzi wengi huiona elimu bora kwa misingi ya michakato ya ufundishaji na kujifunza.

Katika utoaji wa elimu bora utafiti ulisisitiza kuwa wadau wote wanaweza na inabidi wahimizwe kujihusisha kutoa elimu bora yenye ufanisi kupitia maeneo yao ya kazi. Taarifa ilitilia mkazo kanuni za mwongozo zifuatazo ikisisitiza kuwa wadau wote ni lazima waendelee:

- kuhusika katika maendeleo na mabadiliko yanayoendelea ya dira ya pamoja ya elimu bora
- kutilia mkazo msingi wa kufundisha na kujifunza
- kushirikiana na kujenga mifano mingi ya utendaji bora
- kujisikia kuwa na mamlaka na mchango wao kutambuliwa na kuthaminiwa

Washiriki wa utafiti walizingatia vipengele vifuatavyo kuwa muhimu kwa elimu bora itakayotolewa Zanzibar kote:

- mtaala unaowapa wanafunzi:
  - stadi na ujuzi wa ajira
  - uwezo na sifa za msingi kwa uraia bora na mafunzo ya kudumu.
- walimu wenye uwezo katika:
  - kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia
  - kutumia njia za kufundishia zinazowasaidia wanafunzi kupata maana, kutatua matatizo na kuyatumia mafunzo.
- walimu wanaojituma na wenye hamasa
- ushirikiano imara kati ya skuli na jamii zinazozizunguka pamoja na kamati za skuli ili kuhakikisha ushiriki kamili wa wazazi na jamii katika maisha ya skuli
- uwiano kati ya madarasa, walimu na vipindi kwa kila somo
- nyenzo za kufundishia na kujifunzia za kutosheleza
- uratibu kati ya huduma za mafunzo mbalimbali na ufuatiliaji.

## Walimu wakuu fanisi

Washiriki wa utafiti walizipa umuhimu sifa binafsi zifuatazo na matendo ya mwalimu mkuu fanisi.

Walimu wakuu fanisi:

- Hujenga mahusiano madhubuti na jamii inayoizunguka skuli na kamati za skuli.
- Hufanya kazi kwa ufanisi na wafanyakazi wenzake na jamii ili kutengeneza dira ya elimu bora ya pamoja na mipango ya njia za utekelezaji ili kuyatimiza malengo haya.
- Wanajiamini na wana stadi za kuhakikisha kuwa timu yao inatekeleza mipango.
- Anaongoza katika kusaidia maendeleo ya kitaaluma ya walimu. Anatambua mahitaji ya maendeleo ya walimu na kuwezesha fursa za kuendelea kujifunza ikiwa ni pamoja na mafunzo na ushauri kazini.
- Huwapa motisha walimu, kuwatambua, kuwasifu na kufahamishana nao utendaji bora na kutetea hadhi ya ualimu katika jamii.

## Hatua za kuimarisha kipindi cha mpito toka kwenye wajibu wa usimamizi kwenda katika uongozi

Ili Walimu wakuu watoke kwenye wajibu wa usimamizi zaidi kwenda kwenye uongozi, washiriki wa utafiti wameonyesha haja ya kuwepo yafuatayo:

- Muundo imara au dira ya ubora unavyoonekana uwepo katika kiwango cha taifa ili kuwaongoza Walimu wakuu wanapoandaa dira na mipango ya kutoa elimu bora.
- Mafunzo ya uongozi kuwawezesha Wakuu kutengeneza mpango na kuutekeleza.
- Wakuu kuwa na mamlaka zaidi ya kuleta mabadiliko, wakisaidiwa na
  - wajibu, majukumu, mifumo ya uwajibikaji na taratibu vilivyoelezwa waziwazi
  - mifumo ya WEMA na jamii ikiwasaidia Wakuu kimatendo ili watumie mamlaka yao ipasavyo.
- Hadhi ya Wakuu kuimarishwa sawa na majukumu na mamlaka mapya ikiwa pamoja na michakato ya uajiri, malipo ya mishahara na maendeleo ya kazi.
- Kutilia mkazo zaidi mafunzo ya skuli nzima ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya skuli nzima, kauli za dira na elimu bora.
- Kutilia mkazo zaidi utamaduni kujali/kutambua kuwa utambuzi ni sehemu muhimu ya michakato ya uwajibikaji.
- Michakato ya kuimarisha michango ya Wakuu katika uundaji sera na utoaji huduma inahakikisha kuwa Wakuu wanafanya kazi kama wawakilishi wa WEMA.

# Mapendekezo ya kuimarisha wajibu wa uongozi wa Mwalimu Mkuu

Katika kiwango cha jumla taarifa kamili inaweka mapendekezo 69 kwa ajili ya WEMA, Ukaguzi, watoa huduma za mafunzo Kazini na kabla ya kuanza kazi, Walimu wakuu, walimu na Kamati za Menejimenti ya Skuli. Muhtasari huu umeyaunganisha mapendekezo haya katika maeneo makuu yafuatayo:

1. Fursa za kutengeneza dira ya pamoja ya elimu bora zinaongezwa:
   - WEMA inaongoza mijadala ya kitaifa ili kuimarisha dira ya pamoja ya elimu bora na kuendelea kufahamishana mifano ya elimu bora kupitia vyombo vya habari
   - walimu wakuu hufanya kazi na wafanyakazi wenzao na jamii ili kutengeneza dira za pamoja za elimu bora zinazotekelezeka, ambazo huonyesha elimu bora inavyopasa kuwa katika kiwango cha darasa.
2. Wajibu wa Walimu wakuu unarasimishwa kama nafasi rasmi pamoja na:
   - maelezo ya kazi yakieleza stadi, majukumu, viwango vya mamlaka na menejimenti ya karibu
   - upangwaji kazi uliofanywa kupitia michakato rasmi ya uajiri
   - malipo yanayohusiana na viwango vya malipo vilivyozingatia viwango vya majukumu.
3. Mifumo ya tathmini inaanzishwa ili kufanya ufuatiliaji na kusaidia utendaji wa Walimu wakuu na walimu:
   - walimu wapya wenye sifa stahiki kuwa katika kipindi cha majaribio na tathmini ya kuendelea
   - walimu wakuu kuongoza tathmini za walimu
   - kamati ya Uongozi wa Skuli hutoa msaada wa ziada katika kufuatilia mahudhurio ya walimu, utekelezaji wa mtaala na utendaji wa wanafunzi.
4. Programu ya mafunzo ya uongozi wa skuli za majaribio zilizoteuliwa, zikiwemo mafunzo ya vitendo katika mambo ya msingi ya skuli, zinaanzishwa na zipo kwa skuli zote.
5. Walimu wakuu wanatambua na kuwezesha matakwa ya walimu ya maendeleo ya kitaalamu, wakitoa msaada siku za mafunzo ya skuli nzima ambayo huhudhuriwa na wafanyakazi wote.
6. Walimu wakuu wa hushiriki katika maelekezo ya wajibu wa uongozi na shughuli za maendeleo ya kitaalamu; ikiwemo kufundishana na kupeana ushauri kupitia mikutano ya vikundi ambapo hubadilishana mawazo juu ya utendaji bora na ufumbuzi wa masuala ya kila siku kujulikana.
7. Walimu wakuu na WEMA wanaendelea kukuza utamaduni wa kuthamini, wakifurahia ufundishaji na utendaji bora kwa kupeana taarifa ya mtu mmoja mmoja, kushirikiana utendaji bora kati ya skuli na skuli, kuonyesha kazi na machapisho katika vyombo vya habari.
8. Walimu wakuu hufanya kazi na wafanyakazi wenzao katika ngazi ya skuli na ya jamii kuunda na kutekeleza mpango wa miaka miwili wa maendeleo ya skuli unaotilia mkazo jinsi ya kuboresha ufundishaji na kujifunza maskulini.
9. Mabaraza ya wawakilishi kwa walimu wakuu yanaanzishwa katika ngazi ya chini na ya Taifa ili kuwezesha uimarishaji wa sera kupitia michango ya Wakuu, kuimarisha utekelezaji na kuwasaidia Wakuu kufanya kazi kama wawakilishi wa WEMA

Ni matumaini ya mwandishi kwamba mapendekezo haya yatawezesha kukuza zaidi elimu bora Zanzibar kwa njia ambayo itatendea haki malengo ya wanafunzi ya kujiendeleza na kujituma kwa wale wanaohusika katika elimu Zanzibar

Carlton House, 27A Carlton Drive
Putney, London, SW15 2BS, UK.

+44 (0) 20 8780 7500
www.vsointernational.org

VSO is a registered charity
in England and in Wales (313757)
and in Scotland (SC039117).

Cover image © VSO/Martin Brown,
Yasmin Ajmal Published 2011

Ministry of Education and
Vocational Training, Airport
Road, Mazizini, Zanzibar

VSO Tanzania, Plot #997
Off Chole Road, Msasani,
Dar es Salaam, Tanzania

t +255 (0) 22 26 000 72/
f +255 (0) 22 26 000 66
vsotanzania@vsoint.org

**VSO Bahaginan**
www.vsobahaginan.org.ph

**VSO Netherlands**
www.vso.nl

**VSO Ireland**
www.vso.ie

**VSO UK**
www.vso.org.uk

**VSO Jitolee**
www.vsojitolee.org

**CUSO-VSO**
www.cuso-vso.org

Programme undertaken with the financial support of the Government of Great Britain and the Government of Canada through the Department of International Development and the Canadian International Development Agency.